CREATING HOPE IN CONFLICT:

A HUMANITARIAN GRAND CHALLENGE

Ombi la Mapendekezo ya mradi

Mai 21, 2019

USAID FROM THE AMERICAN PEOPLE
UKaid
Ministry of Foreign Affairs of the Netherlands
WITH SUPPORT FROM Grand Challenges Canada® Grands Défis Canada

Muhtasari wa Utendaji

Leo, zaidi ya watu milioni 201 wanahitaji msaada wa kibinadamu. Mamilioni ya watu walio hatarini zaidi katika maeneo yenye mapigano kwa sasa hawafikiwi na usambazaji wa kawaida wa msaada wa kibinadamu. Kadri ya urefu, utata wa mapigano ya askari yanvyotokea mara kwa mara, huwa inaongezeka kuwa ngumu zaidi kuwafikia watu walioathirika katika maeneo ambayo sio salama na msaada wa kibinadamu wa kuokoa maisha na kuboresha maisha.

Wakala wa Marekani wa Maendeleo ya Kimataifa Ofisi ya Msaada wa Maafa ya Kigeni ya Marekani (USAID/OFDA), Idara ya Uingereza ya Maendeleo ya Kimataifa (DFID), Wizara ya Mambo ya Nje ya Uholanzi na Grand Challenges Canada wamezindua Kujenga Matumaini kwenye Mapigano (Creating Hope in Conflict): A Humanitarian Grand Challenge. Shauri hili linatafuta kufadhili na kuharakisha ufumbuzi ambao huwezesha msaada wa kuokoa maisha au msaada wa kuboresha maisha ili kuweza kuwafikia watu ambao wapo hatarini zaidi kudhurika na ambao ni vigumu sana kuwafikia katika majanga ya kibinadamu yaliyosababishwa na mapigano ya kivita.

Hususan, tunatafuta uvumbuzi wa kuishirikisha sekta binafsi na kuhusisha mchango kutoka katika jamii zilizoathirika ili tuweze kufanya, uzalishaji wa maji safi wa ndani na kuondoa maji taka, kuzalisha umeme, kutoa taarifa za kuokoa maisha, kusambaza vifaa vya afya na huduma ili kuwasaidia watu walioathirika na mapigano.

Ombi hili la Mapendekezo ya mradi litafadhili takriban miradi 25 ya mitaji hadi dola za Kanada $250,000 CAD, pamoja na usaidizi wa msingi wa uharakishaji, kwa kipindi cha zaidi ya miezi (24) ishiri na nne. Ili kupokea ufadhili wa mtaji, waombaji lazima waonyeshe wazi uhusiano wa uwezekano, au waeleze fursa za uwezekano wa kushirikiana na sekta binafsi. Maombi ya Mtaji yanahimizwa ili kudhihirisha uhusiano tarajiwa na sekta binafsi kwa (lakini haikomei kwa): kumwongelea mbia wa hivi sasa au tarajiwa wa sekta binsfsi, mbinu inayoegemea kwenye soko, mpito wa kimatukio kwa mbia mahalia, biashara endelevu au suluhisho la kwenye soko. Mwisho wa tuzo ya mitaji, wavumbuzi ambao wameonyesha wazi ushahidi wa fikra ya wazo, kuanzisha mpango wa kipimo na uendelevu, na kupata ahadi za kuvutiwa kutoka kwa washika dau na washirika wanaweza kualikwa kuomba ufadhili wa programu ya TransitionToScale.

Ombi hili la Mapendekezo ya mradi pia litafadhili hadi miradi 5 za uvumbuzi wa Transition To Scale wa hadi dola za Kanada $1,000,000 CAD, pamoja na usaidizi wa uharakishaji, kwa kipindi cha zaidi ya miezi (24) ishirini na nne, kwa ajili ya kurekebisha, kujaribu na kutekeleza ufumbuzi uliogunduliwa ambao umetimiza ushahidi wa wazo husika.

Maombi ya ufadhili wa Transition to Scale yanapaswa kudhihirisha ushiriki, ushirikiano na/au mbinu zilizoundwa na sekta binafsi katika ubunifu, tathimni au utekelezaji wake, na yanahitajika ii kuwa na fedha sawia (fedha taslimu/thamani sawa na fedha taslimu). Watendaji wa sekta binafsi mara nyingi ni wafanisi wa aina yake katika kuzalisha bidhaa kwa haraka na unafuu wa huduma ambazo haziwezi kusambazwa kwa njia za kawaida za msaada wa kibinadamu.

Timu za miradi zilizofaulu zitajumuisha wote watu binafsi ambao wanaelewa maudhui hio ya aina yake ya migogoro iliyosababishwa na vita, na watu ambao wanaweza kuanzisha, kujaribu, kurekebisha na kuhamia kupima uvumbuzi wao ili kuleta athari ya mabadiliko kwa watu katika migogoro iliyosababishwa na vita.

MUDA WA MWISHO WA MAOMBI: MAOMBI YANAPASWA KUPOKEWA SIO ZAIDI YA ALHAMISI, JULAI 16, 2019, SAA 11:00 A.M. MAJIRA YA MASHARIKI YA AMERIKA YA KASKAZINI (15:00 GMT).

Maombi na Barua za kueleza Nia LAZIMA yatumwe kupitia Lango la Jumuiya ya Grand Challenges Canada (gcc.fluxx.io).

Ili kuweza kuingia kwenye Tovuti husika, waombaji wanapaswa kwanza kuunda akaunti kwa kutumia kiungo kifuatacho: Unda akaunti. Mara tu taarifa yako ikichakatwa, utatumiwa barua pepe yenye maelezo ya kuingilia ili uweze kuingia kwenye Lango na kutuma maombi yako. Kwa usaidizi wa kiufundi, tafadhali wasiliana na fluxxsupport@grandchallenges.ca.

Ukimaliza kuunda akaunti yako, tafadhali subiri angalau siku (1) moja ya kazi ili Grand Challenges Canada waweze kushughulikia ombi la akaunti yako. Hivyo basi, tunashauri kuunda akaunti sio zaidi ya Julai 5, 2019.

Orodha ya Yaliyomo

MUHTASARI WA UTENDAJI ..... **II**

1. UTANGULIZI **5**

2. MBINU **5**

2.1 Changamoto Kubwa (The Grand Challenge) 5
2.2 Maeneo ya Kuzingatia 5
2.4 Watu Walengwa 10
2.5 Ufadhili Uliopo 10
2.6 Mkazo kwenye Matokeo 12
2.7 Jukumu la Sekta Binafsi 12
2.8 Kipimo na Uendelevu 13
2.9 Uendelevu wa Mazingira, Usawa wa Kijinsia, Haki na Binadamu na Ujumuishwaji 14
2.10 Upatikanaji Kimataifa, Upatikanaji wa Takwimu na Maadili 14
2.11 Usimamizi wa Hatari, Usalama, Kupambana na Ugaidi, Kupambana na Rushwa, Kupinga Rushwa 15
2.12 Mambo Ambayo Hatutayafadhili 15

3. SHUGHULI NA VITU VYA KUWASILISHA **15**

4. SHERIA NA MIONGOZO **16**

4.1 Vigezo vya Sifa 16
4.2 Maelekezo ya Maombi 17
4.3 Ratiba za Muda wa Maombi 19
4.4 Mchakato wa Mapitio 19
4.5 Vigezo vya Tathimini 21
4.6 Vigezo vya Tathimini– kwa ajili ya kujiridhisha kuhusu maombi ya Transition to Scale 22
4.7 Vigezo vya Kifedha na Gharama Stahiki 23
4.8 Vigezo vya Malipo 23
4.9 Ukaguzi 24
4.10 Nyaraka za Kuwakilisha na Ilani ya Faragha 24
4.11 Hati ya idhini 25
4.12 Haki za Uvumbuzi 25
4.13 Upatikanaji wa Takwimu 25
4.14 Haki za Grand Challenges Canada 26
4.15 Hakika za Utafiti 27

KIAMBATISHO A **28**

1. Utangulizi

Leo, zaidi ya watu milioni 201 wanahitaji msaada wa kibinadamu. Mamilioni ya watu walio hatarini zaidi katika maeneo yenye mapigano kwa sasa hawafikiwi na usambazaji wa kawaida wa msaada wa kibinadamu. Kadri ya urefu, utata wa mapigano ya askari yanvyotokea mara kwa mara, huwa inaongezeka kuwa ngumu zaidi kuwafikia watu walioathirika katika maeneo ambayo sio salama na msaada wa kibinadamu wa kuokoa maisha na kuboresha maisha.

Mashirika ya kimataifa ya misaada yanakabiliwa na changamoto katika kufikisha misaada ya kibinadamu kwenye maeneo yaliyoathiriwa na vita, ikiwa ni pamoja na kunyimwa ufikio, miundombinu mibovu, vuzuizi vya kisiasa, upindishwaji wa misaada, ufisadi, changamoto za kitamaduni, uratibu duni na vitisho vya ukatili. Watumishi wa ndani mara nyingi ni bora zaidi kuwekwa ili kuwafikia watu walioathirika katika mazingira yasiyo salama, lakini wanapungukiwa na ufadhili au zana, au uwezo wa kutoa msaada katika maeneo ambayo ni vigumu kufikia.

Kadri ambavyo kiwango cha dharura za kibinadamu kinaendelea kukua kwa kipimo kinachovuka uwezo wa mbia au sekta yoyote kuwa na mwitikio na ufadhili wa misaada ya kibinadamu hushindwa kukidhi mahitaji yanayoongezeka, njia mpya za kufikiri na kufanya kazi pamoja ni mambo muhimu. Kushirikiana na sekta binafsi ni muhimu katika kuanzisha mbinu mpya ili kuzikamilisha mbinu za kawaida za usambazaji wa msaada wa kibinadamu. Sekta binafsi mara nyingi ni fanisi sana katika kupima ufumbuzi endelevu na katika kuongeza kasi, ubora na unafuu wa kusambaza au kutengeneza bidhaa na huduma, kutumia tena bidhaa na kugharamia au kuanzisha ufumbuzi bunifu.

Ili kuboresha msaada katika maafa yaliyosababishwa na vita, Wakala wa Marekani wa Maendeleo ya Kimataifa Ofisi ya Msaada wa Maafa ya Kigeni ya Marekani (USAID/OFDA), Idara ya Uingereza ya Maendeleo ya Kimataifa (DFID), Wizara ya Mambo ya Nje ya Uholanzi na Grand Challenges Canada wameanzisha Kujenga Matumaini kwenye Mapigano (Creating Hope in Conflict): A Humanitarian Grand Challenge.

2. Mbinu

2.1 CHANGAMOTO KUBWA (THE GRAND CHALLENGE)

Tunatafuta uvumbuzi wa kuokoa maisha au wa kuboresha maisha ili kuwasaidia watu ambao wapo hatarini zaidi au ni vigumu sana kuwafikia walioathirika na majanga ya kibinadamu yaliyosababishwa na mapigano. Vumbuzi hizi zitahusisha muungano na sekta binafsi na mawazo kutoka katika jamii zilizoathiriwa na janga la kibinadamu ili kutoa huduma ya maji safi ya kunywa, usafi, nishati, taarifa zinazookoa maisha, au vifaa na huduma za afya ili kuwasaidia watu walioathiriwa na machafuko.

2.2 MAENEO YA KUZINGATIA

Humanitarian Grand Challenge inalenga kushughulikia mahitaji ya shida kali zaidi katika maeneo yaliyoathirika na mapigano mahitaji ambayo yana uwezekano wa kutatuliwa na uvumbuzi kwa eneo moja au maeneo zaidi kati ya yafuatayo: (1) maji safi na kuondoa maji taka; (2) umeme; (3) taarifa za kuokoa maisha; or (4) vifaa vya afya na huduma za afya. Uvumbuzi lazima uwezeshe ufumbuzi wa ndani, uhudumie mahitaji ya ndani na mapungufu ya usambazaji, kushinda vikwazo vya kawaida vya usambazaji katika mazingira ya mapigano, au kuongeza kipindi cha muda na unafuaa wa njia za

sasa za usambazaji wa kibinadamu. Tunakaribisha pia vumbuzi zinazosaidia kudumisha huduma na miundombinu, ili kuepuka uharibifu zaidi.

Vumbuzi zinazopendekezwa zinapaswa kuelezea waziwazi tatizo walilolibaini, visababishi vya msingi vya tatizo mahsusi, na namna huo uvumbuzi uliotambuliwa utashughulikia kisababishi kimoja au zaidi. Vumbuzi zilizo katika mchakato au mbinu (k.m. zinazozoeza mbinu ya sekta binafsi katika muktadha wa kibinadamu) zinazokaribishwa sana.

Maeneo ya kuzingatia yamefafanuliwa kwa undani hapo chini.

Maji Safi na Kuondoa maji taka

Ugavi na Ubora wa Maji

Maji salama ni muhimu kwa ajili ya kudumisha afya ya watu na jumuiya pamoja na utendaji wa huduma za msingi, kama vile huduma ya afya. Kwa mfano, virutubisho vya lishe vya chakula cha msaada vinahatarishwa pale maji yaliyochafuliwa na viini yanaposababisha magonjwa au maradhi. Tunakaribisha mawazo, teknolojia, michakato na mbinu za kijasiri ambazo:

1. *Zinaongeza upatikanaji na ufikio wa maji katika maeneno ya machafuko:* upatikanaji na ufikiaji huathiriwa na mapato yanayobadilika na ruwaza za matumizi kwenye ngazi za nyumbani, jumuiya na manispaa; ruwaza mpya za msongamano wa watu; upatikanaji mdogo wa chanzo cha umeme (k.m. kukatika-katika au kukokuwepo umeme, ongezeko la bei ya mafuta); usalama; na vitendeshi vya tabianchi kama vile ukame au mafuriko. Hata kama maji yanapatikana, watu walioathiriwa na machafuko wanaweza kuhitajika kutembea umbali mrefu, mara nyingi wakihatarisha usalama wao binafsi, ili kufikia chanzo cha maji. Kubeba maji kwa kutumia malori ili kukidhi mapengo ya ugavi ni aghali na kunahatarisha kushambuliwa.
2. *Zinawezesha ongezeko la utendaji wa mifumo iliyopo*: ufikio wa vifaa na vipuri vipya ili kurekebisha mifumo iliyoharibika/iliyoharibiwa au zinazowezesha matengenezo ya msingi mara nyingi ni chache; kuna ukosefu wa ufikio wa bidhaa za kutibu maji; ukosefu wa vifaa rahisi vya kufuatilia ubora wa maji; na ukosefu wa watendaji mahiri wa kuendesha mifumo mikubwa ya maji. Kuanguka (au ukosefu wa) mifumo ya udhihiti ili kufuatilia huduma za maji za sekta binafsi (kubeba maji kwa malori, maji ya kopo, n.k.) nayo inaathiri ufikio wa maji salama.
3. *Zinashughulikia ufikio unaodhibitiwa na unaozuiwa kutokana na usalama:* ukatili na ukosefu wa usalama huzuia utoaji na ufuatiliaji wa maji salama.

Usimamizi wa Maji safi/Taka na Mazingira

Watu wanaoathiriwa na machafuko wana uwezekano mkubwa wa kupata magonjwa kutokana na uhaba wa usafi wa mazingira na usimamizi wa taka. Watoto, wazee na watu wanaosumbuliwa na matatizo mengine ya kiafya ndiyo hasa walio hatarini. Kuboresha usafi wa mazingira mara nyingi ni jambo muhimu la kushughulikia suala la utapiamlo. Tunakaribisha mawazo, teknolojia, michakato na mbinu za kijasiri ambazo:

1. *Zinaboresha ufikio wa usafi salama wa mazingira:* Viwango vya msingi vya taarifa hafifu za usafi wa mazingira huzorota zaidi wakati wa machafuko kwa kupoteza makazi na ruwaza mpya za msongamano wa watu, hasa kwa kaya zinazowahifadhi wasikwao. Sehemu zilipojengwa vyoo mara nyingi huhatarisha usalama na ulinzi, hasa kwa wanawake, wasichana na watu wenye ulemavu.
2. *Zinazoeza vizuri tabia za usafi wa mazingira:* desturi na miiko iliyopo ya kitamaduni inaweza kukinzana na ruwaza mpya za maisha, ikiwemo kuzoea kutumia choo, bafu, au huduma nyingine ya umma.
3. *Zinashughulikia changamoto za miundombinu ya usafi za mazingira:* katika kambi zenye msongamano au maeneo ya mjini hakuna sehemu nyingi kujenga miundombinu ya kutosha ya usafi wa mazingira ili kukidhi viwango vya kijitabu cha SPHERE.[1] Ukosefu wa huduma hizi unaweza kusababisha jumuiya kurejea tabia ya kujisaidia nje, kwa kuwa hakuna chaguzi nafuu au sahihi kwao.
4. *Zinaunda au kuboresha mifumo ya kusimamia taka:* mifumo ya kusimamia taka katika mazingira ya machafuko ni michache, haisimamiwi vizuri, au haipo kabisa. Tunatafuta suluhisho mpya au zilizoboreshwa za kutupa taka, ikiwemo kinyesi, usimamizi wa taka za nyumbani na za wanyama.

Nishati

Tunakaribisha mawazo, teknolojia, michakato na mbinu za kijasiri ambazo:

1. *Zinaunda vyanzo nafuu, safi na vya kuaminika vya umeme:* Ugavi wa umeme katika mazingira ya machafuko mara nyingi si wa kuaminika, ni duni, ni aghali, unaweza sana kushambuliwa, na hautoshi kukidhi mahitaji ya watu walioathiriwa pamoja na miundombinu inayohitaji sana nishati (kama vile mashule, hospitali, masoko), maeneo yalioungwanishawa au yasiyoungwnaishwa na gridi.
2. *Zinaunga mkono wauzaji mahalia wa vifaa vya umeme na huduma za ukarabati/matengenezo:* Kuna uhitaji wa wauzaji mahalia zaidi wa vifaa vya umeme na huduma za ukarabati/matengenezo katika mazingira yenye machafuko.
3. *Zinabaini vizuri uhitaji na matumizi ya umeme:* kuna ukosefu wa taarifa kuhusu uhitaji wa nishati, matumizi, na gharama katika mazingira yenye machafuko ambayo yanafanya kuwa ngumu kwa huduma za nishati kukidhi wigo mpana wa mahitaji, kuanzia majumbani mpaka kwa watoa huduma.

Taarifa za kuokoa maisha

Tunakaribisha mawazo, teknolojia, michakato na mbinu za kijasiri zinazotoa na/au kuboresha ufiko wa taarifa zinazookoa maisha kwa:

[1] https://www.spherestandards.org/handbook-2018/

1. *Kushughulikia changamoto za miundombinu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA):* muunganisho wa intaneti na huduma za WiFi hazitabiriki au hazipo kabisa katika nchi zilizoathiriwa na machafuko na katika mazingira ya kambi.
2. *Kuboresha ulinzi wa kibinadamu:* vumbuzi zinahitajika ili kuongeza ulinzi wa watu walioathiriwa dhidi ya madhara ya kimwili, pamoja na ulinzi wa kidijitali wa watu na wafanyakazi wa masuala ya kibinadamu.
3. *Kuongeza umahiri wa kidijitali, ufikio na utumiaji wa vifaa:* marudio na aina ya ufiko wa vifaa huweza kutofautiana katika mazingira yenye machafuko, pamoja na unafuu wa vifaa na viwango vya umahiri wa kidijitali. Ufikio wa vifaa mara nyingi pia hutegemea na jinsia, huku ufikio/umiliki wa wanawake ukiwa mdogo sana.
4. *Kuboresha mawasiliano ya pande zote mbili:* upungufu wa muda na rasilimali huelekezwa kwa mawasiliano ya pande zote mbili kati ya watendaji wa masuala ya kibinadamu na jumuiya zilizoathiriwa wanazotaka kuzihudumia. Mara nyingi mawasiliano ya pande zote mbili hukosa tanzi za mrejesho.
5. *Kuwezesha ukusanyaji bora wa takwimu na uchambuzi kwa ajili ya ufanyaji maamuzi na uwajibikaji:* Tathmini za haraka, sahihi na wakilishi, mahitaji ya watu kwa kawaida ni za juujuu na hushindwa kutoa takwimu zenye tija au ni za kina sana na zinazochukua muda mwingi na hushindwa kuwa na faida kwa wakati unaofaa. Kuna mabadiliko pia katika kuunganisha matokeo kutoka mbinu za tathmini ya ubora na tathmini ya madhara.

Huduma na Vifaa vya Afya

Msaada wowote kwa vituo na huduma unapaswa kuzingatia kanuni za kibinadamu na haupaswi kujumuisha mifumo ya ubaguzi[2]. Msaada unapaswa pia kuzingatia maboresho ya huduma za rufaa za huduma za msingi za afya kwa kutumia vituo mahalia. Suluhisho zinapaswa pia kuzingatia uwekaji mipango ya dharura na utayari kwa ajili ya mwitikio wa mapema kwa upanuzi wa uhitaji na mzigo wa matukio. Tunakaribisha mawazo, teknolojia, michakato na mbinu za kijasiri ambazo:

1. *Kuwezesha au kuboresha uzalishaji mahalia wa zana za afya na lishe:* Zana za afya na lishe zinaweza kutokuwepo au inaweza kuchukua muda mrefu kwa zana hizo kuwasilishwa, na kuna njia chache kwa jumuiya zilizoathiriwa kuzalisha zana muhimu na za ubora wa juu na zilizo salama kimahalia, au kuua viiini na kutumia tena baadhi ya rasilimali pale inapowezekana.
2. *Kuboresha usimamizi wa bidhaa za tiba na lishe:* mazingira yenye machafuko yana minyororo mirefu na mara nyingi iliyo aghali ya ugavi, ambayo pia inaweza kukosa uwazi na uwajibikaji. Vizuizi vya udhibiti vinaweza kuzuia au kuchelewesha uwasilishaji wa ugavi wa tiba na lishe. Usafirishaji na uhifadhi sahihi unaweza kuvurugwa. Dawa katika mazingira yenye machafuko mara nyingi ni zenye ubora duni/usiofahamika.
3. *Kuwaunga mkono watoa huduma za afya:* kuna uhaba wa ufikio wa mafunzo ya ubora wa juu kwa watoa huduma za afya. Palipo na fursa, kuwabakiza wataalamu wa huduma ya afya inaweza kuwa changamoto kwa kuwa wataalamu wanaweza kulazimika kukimbia. Ukosefu wa kuaminiana kati ya watoa huduma za afya na jumuiya ni changamoto nyingine inayoweza

[2] Wakati mwingine zinaitwa “Kujificha katika handaki”. Tazama “Baki na Wasilisha, OCHA” kwa taarifa zaidi.

kutokea. Kuna uhitaji wa kuwawezesha na kuwalinda wafanyakazi wa huduma ya afya katika maeneo yenye machafuko na kuwezesha uhamishaji wa majukumu ili kutoa huduma bora, kama vile uchunguzi sahihi na lishe.

4. *Kuboresha vituo na huduma za afya:* kuna upungufu wa hospitali na kliniki kwenye mazingira yenye machafuko, jambo linalozoroteshwa zaidi kwa kuwa sehemu zinazolegwa kwa mashambulizi. Vituo vilivyopo havina vifaa muhimu na ukarabati. Tunahimiza njia mpya za kutoa misaada – katika mazingira mapya na ya tofauti.
5. *Kuboresha Uwezo wa Mwitikio wa Mlipuko wa Dharura:* Milipuko ya magonjwa inayogusa maeneo makubwa inaweza kutokea zaidi kwenye maeneo yenye machafuko ambapo miundombinu ya maji, usafi wa mazingira na usafi wa mwili inakuwa imezidiwa, zana za uchunguzi ni chache, na dawa ni haba. Kupoteza makazi kwa watu wengi, pamoja na uhaba wa watoa huduma za afya, na uharibifu wa miundombinu ya afya hupelekea ongezeko la ukubwa na ukali wa milipuko kwa milipuko ambayo mara nyingi huzuiwa kwa chanjo.
6. *Kushughulikia mahitaji yanayopewa kipaumbele:* Magonjwa yasiyo ya kuambukizwa yanazidi kuwa changamoto kubwa za kiafya katika mazingira yenye machafuko. Kwa mfano, unyanyapaa na utata wa matibabu huweza kupelekea matibabu duni ya maradhi ya akili. Mazingatio yanapaswa kutolewa kwa uendelevu wa huduma za afya katika awamu ya baada ya dharura.
7. *Kuhakikisha usalama wa watoa huduma za afya*. Kuna uhitaji wa kujumuisha michakato ya kuripoti na kuwawajibisha waanzilishi wa machafuko kwa kukiuka Sheria za Kimataifa za Masuala ya Kibinadamu.

Kulingana na ubora wa barua za maombi ya mradi zinazopokewa, Humanitarian Grand Challenge inabakiza haki ya kupunguza malengo hadi moja au zaidi ya maeneo yaliyotajwa hapo juu. Maombi ya pendekezo la mradi ambayo yanazungumzia zaidi ya sekta moja yanakaribishwa sana.

2.3 KUTAFSIRI UVUMBUZI

Tunatafsiri uvumbuzi kama mawazo ya kijasiri yenye uwezekano wa kufanya mageuzi makubwa ya namna ambavyo suluhisho zinazookoa maisha na zinazoboresha maisha zinawafikia na kuwasaidia watu wengi walio katika mazingira hatarishi waliokumbwa na machafuko. Uvumbuzi unamaanisha kulikabili tatizo kwa njia mpya na tofauti mbali na jitihada zilizopo.

Tafsiri yetu ya uvumbuzi inajumuisha kuyajaribu mawazo yaliyopo kwa muktadha mpya. Jambo fulani linalofanya kazi katika muktadha ulio thabiti ambalo halijawahi kujaribiwa katika mazingira yenye mechafuko, linaweza pia kufikiriwa kwa ufadhili. Katika masuala haya, suluhisho linapaswa kudhihirisha uelewa yakinifu wa mazingira yenye machafuko na lina uwezekano wa kushungulikia kizuizi mahsusi kilichopo ambacho kinazuia msaada wa kibinadamu katika maeneo ya machafuko huku likidumisha kanuni za kibinadamu.

Uvumbuzi Fungamano

Miradi inategemewa kutumia mbinu ya Uvumbuzi Fungamano®, inayofasiliwa kama matumizi ya uvumbuzi wa kisayansi/kiteknolojia, kijamii na kibiashara, kuunda fumbuzi za changamoto ambazo ni ngumu. Mbinu hii haipunguzi faida moja moja za aina hizi za uvumbuzi peke yake, badala yake

zinakazia mahusiano yenye nguvu ambayo yanaweza kupatikana kwa kuunganisha mambo yote matatu. Kwa taarifa zaidi, tafadhali tazama: www.grandchallenges.ca/funding-opportunities/integrated-innovation/).

2.4 WATU WALENGWA

Humanitarian Grand Challenge inalenga kuwasaidia watu ambao ni vigumu kufikiwa kutokana na dharura za kibinadamu zinazotokana na mapigano. Huku tukiwazingatia wakimbizi na wasikwao mahalia kuwa walengwa mahsusi, kipaumbele chetu ni kuhudumia wale wanaoishi kwenye maeneo yenye machafuko. Muktadha tunaochukulia kuwa maeneo yasiyofikika kwa urahisi ni pamoja na, lakini hayakomei katika:

- Afghanistani
- Jamhuri ya Afrika ya Kati
- Iraki
- Libya
- Mali
- Nigeria Kaskazini
- Somalia
- Sudani Kusini
- Syria
- Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo
- Yemeni

Tunahimiza vumbuzi zinazolenga watu waliodunishwa na jamii kwa sababu ya jinsia, ngono, hisia za kingono, dini, umri au kipato, pamoja na watu wenye ulemavu, kundi la watu wachache na watu wasio raia wa taifa lolote.

Tunaunga mkono vumbuzi zinazoimarisha taasisi mahalia, asasi za kiraia, na wasambazaji wa huduma.

2.5 UFADHILI ULIOPO

Mtaji
Lengo la fedha za mtaji ni kujaribu mawazo na mbinu mpya kwenye misaada ya kibinadamu, ili kuamua iwapo ni fanisi ama la. Kufikia mwisho wa kipindi cha ufadhili, miradi iliyopata mtaji inategemewa kuonesha ushahidi (k.m., ushahidi wa dhana), kwenye mazingira yanayodhibitiwa au yaliyozuiliwa, kwamba kuna usaidizi mkubwa kwenye eneo linalolengwa, utegemezi mdogo wa misaada, na/au kupungua kwa vikwazo vingine muhimu vya kupata msaada kutokana na mradi huu, pamoja na kwamba uvumbuzi una uwezekano wa kutekelezwa kwa upana kwenye muktadha mwingine.

Kupitia Ombi hili la Mapendekezo ya Miradi, wabia wa Humanitarian Grand Challenge watatoa fedha za mtaji zinazofikia Dola za Canada 250,000 kwa kila mradi kwa kipindi kisichozidi miezi ishirini na nne (24) Mbali na kufadhiliwa, washindi wanaweza kupata usaidizi wa ziada, kama vile kusaidiwa katika matangazo na kutafuta masoko, kufikia sherehe za kipekee za sekta, wawekezaji na wabia; na msaada wa kawaida wa kuchapuza, fursa za ushauri na kuingia ubia.

Ngazi ya ufadhili inayoombwa inapaswa kuwa ya kutosha ili kuhakikisha utimilifu wa malengo yaliyobainishwa kwenye ratiba ya muda na inapaswa kuwa ya haki kabisa.

Tunategemea kutoa ruzuku za mtaji kwa washindi hadi 25 kupitia Ombi hili la Mapendekezo ya miradi. Kufikia mwisho wa kipindi cha utoaji wa fedha za mtaji, kama ushahidi wa dhana umepatikana, vumbuzi zinaweza kualikwa kutuma maombi kwenye njia ya ufadhili ya mpito wa kupima.

Ili kupokea fedha za mtaji, waombaji wanapaswa kudhihirisha uwezekano wa umuhimu wa au kubainisha uwezekano wa fursa ya kushirikiana na sekta binafsi.

Ufadhili wa Mpito wa Kupima (TTS)
Ushirikiano wa kimkakati unahitajika kwa ajili ya mpito wa kupima na uendelevu wa fumbuzi za uvumbuzi.

Ufadhili linganifu (fedha taslimu) kutoka kwa wabia wa kimkakati kwa shughuli zinazoendeleza ukuaji, maendeleo, mauzo au uasilishwaji wa uvumbuzi (k.m., uzalishaji, usambazaji, uuzaji, mitandao) itatafsiriwa kama kuongezeka kwa dhamira ya mbia. Wengi wa washindi wa ufadhili watahitajika kuwa na ulinganifu wa 1:1 ndani ya kipindi cha ufadhili wa Mpito wa Kupima (TTS); hata hivyo, jambo hili litatathminiwa kwa mujibu wa kesi kwa akesi wakati wa kipindi cha umakini. Wabia wa kimkakati wanaweza kutoa rasiliamali watu na rasilimali nyingine zisizo za kifedha kwa shughuli za mradi; hata hivyo, washindi wa ufadhili hawaruhusiwi kutegemea tu aina hizi za michango ya kikarimu ili kukindhi vigezo vya ulinganifu.

Kupitia Ombi hili la Mapendekezo ya Miradi, wabia wa Humanitarian Grand Challenge watatoa ufadhili wa Mpito wa Kupima hadi kufikia Dola za Canada 1,000,000 kwa kila mradi kwenye ratiba ya muda iliyobainishwa kwa kipindi kisichozidi miezi ishirini na nne (24). Ngazi ya ufadhili iliyoombwa inapaswa kuwa ya kutosha ili kuhakikisha utimilifu wa malengo yaliyobainishwa kwenye ratiba ya muda na inapaswa kuwa ya haki kabisa.

Tunategemea kuwekeza kwenye miradi hadi 5 ya Mpito wa Kupima; inaweza kuwa ni ruzuku, ruzuku zinazopaswa kulipwa, mikopo isiyo na riba, mikopo yenye riba, deni linaloweza kubadilishwa, mikataba ya malipo kulingana na matokeo au mjumuisho wa yote Uchaguzi wa muundo wa uwekezaji unataarifiwa na (i) hatua na njia ya shirika ya kupima (k.m, kwa faida au bila faida), (ii) uwezo wa muundo wa kuvutia vyanzo vya ziada vya mtaji, ikiwa ni pamoja na wabia binafsi, kama wawekezaji wafuatiliaji, (iii) uwezekano wa madhara kwenye matokeo ya afua na kuhusu uendelevu wa shirika, ikihusisha uwezo wake wa kujiendeleza, (iv) dhamira ya kuhimiza urejeshaji wa fedha pale uwekezaji utakua kwa mafaniko na faida.

Wabia wa Humanitarian Grand Challenges wataunga mkono ujengaji wa mahusiano kati ya wavumbuzi waliopata ufadhili pamoja na sekta binafsi, watendaji wa masuala ya kibinadamu na wadau wengine ili kuongeza uwezekano wa mafanikio. Msaada wa kiufundi na ushauri unaweza kutolewa ili kukuza upimaji na uendelevu wa vumbuzi za kibinadamu. Vivyo hivyo, washindi wa ufadhili wanaweza kupata usaidizi zaidi, kama vile kusaidiwa katika matangazo na kutafuta masoko, kufikia sherehe za kipekee za sekta, wawekezaji na wabia; na msaada wa kawaida wa kuchapuza, fursa za ushauri na kuingia ubia.

Utolewaji wa fedha kwa wavumbuzi utategemea na Grand Challenges Canada kupokea fedha kutoka kwa mfadhili/wafadhili wetu.

2.6 MKAZO KWENYE MATOKEO

Matokeo ya mwisho ya nia ya hii Humanitarian Grand Challenge ni **maisha yaliyookolewa na maisha yaliyoboreshwa** ya watu waliothirika na mapigano. Matokeo mengine ya ubora na wingi yanapaswa kukusanywa ili kuonesha kwa ufasaha kabisa matokeo ya uvumbuzi husika.

Kutokana na kwamba matokeo halisi ya vumbuzi yapo katika siku za usoni, maombi ya mradi yanapaswa kujumisha mpango wa namna viashiria vya papo hapo na kipindi cha kati vitakavyofuatiliwa na kutathiminiwa kwa kipindi chote cha mradi husika.

Kwa vumbuzi ambazo hazitafanikwa, inategemewa wavumbuzi wataweza kueleza kwa nini hazikufanikiwa, ili kuweza kuchapuza maendeleo kwenye sekta husika. Kwa kutegemea ufadhili, tunanuia kuwaleta pamoja wavumbuzi mahiri kushirikishana mafunzo na maoni waliyojifunza

Kutoa Taarifa ya Matokeo
Kutoa taarifa ya matokeo ni sehemu muhimu ya uwajibikaji wa mradi kwa wabia wa Human Grand Challenge na wadau wengine muhimu. Wavumbuzi wanapaswa kuzingatia ni namna gani matokeo yatasambazwa ili kuchapuza matokeo, usambaaji na uendelevu wa uvumbuzi. Huku kutoa taarifa ya matokeo kupitia machapisho ya kisayansi inaweza kuwa jambo fanisi, hii haipaswi kuwa lengo la msingi la miradi.

Kwa taarifa zaidi tazama Kiambatisho A.

2.7 JUKUMU LA SEKTA BINAFSI

Kutokana na kipimo cha sasa cha mahitaji ya kibinadamu, changamoto hii ni kubwa sana kwa sekta moja kuifumbua peke yake. Sekta binafsi inaweka mbinu za kupima, kupima kwa ufanisi fumbuzi endelevu, kuboresha kasi, ubora na unafuu wa bidhaa za viwandani na huduma, kurejeza bidhaa na kufadhili fumbuzi za kivumbuzi kunaweza kupelekea kupata fumbuzi zenye ufanisi na matokeo zaidi. Sekta binafsi inaweza kuchangia utaalamu wenye thamani wa kiufundi, usimamizi wa hatari, na upatikanaji wa mitandao na takwimu, na mara nyingi huweza kuwa na uelewa wa kina wa hali mahalia. Kwa mfano, biashara ndogondogo mahalia mara nyingi ni muhimu katika kutoa bidhaa zinazookoa maisha na zinazoboresha maisha pale yanapotokea mapigano ya kutumia sialaha. Wavumbuzi wanahimizwa kuhusisha umahiri wa msingi wa sekta binafsi kwenye muundo wao au kushirikiana na sekta binafsi ili kuongeza nguvu ya matokeo ya vumbuzi zao.

Ili kupokea fedha za mtaji, waombaji wanahimizwa kudhihirisha uwezekano wa umuhimu wa, au kubainisha uwezekano wa fursa ya, kushirikiana na sekta binafsi. Maombi ya Mtaji yanahimizwa ili kudhihirisha uhusiano tarajiwa na sekta binafsi kwa (lakini haikomei kwa): kumwongelea mbia wa hivi sasa au tarajiwa wa sekta binsfsi, mbinu inayoegemea kwenye soko, mpito wa kimatukio kwa mbia mahalia, biashara endelevu au suluhisho la kwenye soko.

Ili kufadhiliwa fedha za mpito wa kupima, unahitajika ushirikiano na sekta binafsi. Wavumbuzi wanapaswa kuwahusisha watendaji wa sekta binafsi wanaoweza kujaza pengo muhimu linalohitajika katika kukuza au kuboresha uvumbuzi wao. Hii inaweza kuhusisha utaalamu wa

kiufundi, chaneli za usambazaji, upatikanaji wa takwimu, uelewa mahalia, msaada wa kifedha, au uwezo au ushirikiano mwingine wa msingi. Katika baadhi ya hali, wabia wa Humanitarian Grand Challenge wanaweza kusaidia upatikanaji wa wabia sahihi kutoka sekta binafsi, ili mradi waombaji wawe wa uwezo wa kuelezea mahitaji yao. Ingawa inapendelewa zaidi, dhamira thabiti ya ushiriki wa sekta binafsi haihitajiki wakati wa kufanya maombi ya mradi.

Sekta binafsi inafasiliwa kama vyombo vinavyopata faida kwenye ngazi mahalia, kitaifa na kimataifa, na hurejelea mashirika na watendaji:

- Vyombo vinavyopata faida, kama vile biashara, mashirika makubwa, au kampuni binafsi
- Taasisi za kifedha, ikiwa ni pamoja na makampuni ya uwekezaji, mifuko ya hisani ya jamii au makampuni ya bima
- Wawekezaji binafsi (watu binafsi au makundi)
- Biashara binafsi au vyama vya sekta husika, ikiwa ni pamoja lakini haiishii tu kwenye chemba za biashara na vyombo kama hivyo.
- Mifuko ya hisani binafsi inayotoa ruzuku au vyombo vya uhisani

Ujumuishwaji wa sekta binafsi kwenye maombi unaweza kuwa ama kupitia ushiriki wa kifedha au uhisani, au ushirikiano

Vyombo vya sekta binafsi navyo pia vinahamasishwa kutuma maombi kwa ajili ya ufadhili.

2.8 KIPIMO NA UENDELEVU

Kwa matumizi ya Humanitarian Grand Challenge, uendelevu unarejelea uwezo wa vumbuzi zilizochaguliwa kuweza kutumiwa kwenye muktadha unaoendelea na wa siku za usoni, na kipimo hurejelea uwezo wa vumbuzi zilizochaguliwa kufikia idadi kubwa kabisa ya watu watakaonufaika kadri iwezekanavyo. Andiko ya miradi inapaswa kuelezea kwa ushawishi ni namna gani miradi yao itafikia kipimo na kuendelezwa. Wavumbuzi wanapaswa kutumia fedha za mtaji kujaribu njia za kipimo na uendelevu, na wanapaswa kuwa na mpango thabiti na dhana iliyothibitishwa ili kuweza kupata ufadhili wa mpito wa kipimo

Waombaji wa Mpito wa Kipimo wanapaswa kuwa tayari na mpango madhubuti wa kipimo na uendelevu, ikiwa ni pamoja na ahadi kutoka kwa wadau na wabia muhimu wanaohitajika ili kuendelea kwenye njia ya kipimo na uendelevu.

Uelewa wa Maafa Yanayotokana na Mapigano
Ili kusaidia kuhakikisha matokeo endelevu kwenye kipimo, ni muhimu kwamba timu za mradi zihusishe watu wenye uelewa wa muktadha mahalia wa kijamii, kisiasa na kuuchumi. Kwa kufanya hivyo, miradi itaweza kushughulikia vizuri zaidi mahitaji ya watu walioathiriwa na kutambua hatari dhidi ya mafanikio ya mradi.

Ushiriki wa Wadau
Watu walioathiriwa na mapigano na wale ambao hatimaye watafanya maamuzi kuhusu matumizi ya ufumbuzi, kama vile mashirika ya kibinadamu (mahalia, kitaifa au kimataifa), mashirika ya Umoja wa Mataifa, vyombo vya Msalaba Mwekundu au waitikiaji wasio wa kawaida (makundi ya kiimani, makundi ya jamii mahalia, sekta binafsi) wanategemewa kushirikishwa tangu mwanzo na katika kipindi chote cha uhai wa mradi. Mawazo na ushirikishwaji wa aina hii ya mashirika kwenye

kipindi chote cha uhai wa mradi ni jambo muhimu, kwa kuwa watajumuishwa kwenye mchakato wa tathimini. Hii itasaidia kuhakiksha kwamba ufumbuzi utakuwa tayari kwa uasilishwaji wa awali na matumizi ya baadaye, na kupekelea matokeo makubwa. Vivyo hivyo, wadau wanaweza kutoa uelewa juu ya jamii yao na kutambulisha mambo muhimu kwa ajili ya mafaniko ya mradi.

2.9 UENDELEVU WA MAZINGIRA, USAWA WA KIJINSIA, HAKI NA BINADAMU NA UJUMUISHWAJI

Wavumbuzi watakaopata ufadhili chini ya hii Humanitarian Grand Challenge wanapaswa kutii sera za Grand Challenges Canada za Uendelevu wa Mazingira, Uswa wa Kijinsia, Haki za Binadamu na Ujumuishwaji.

Uendelevu wa Mazingira
Waombaji wanapaswa kudhamiria kuhakikisha kwamba uvumbuzi wao hautakuwa na madhara kwenye mazingira, ikihusisha lakini haiishii tu kwenye madhara ya muda mrefu na yanayokua. Ikiwezekana, wavumbuzi wanapaswa kujumuisha matokeo chanya ya kimazingira kwenye kipindi chote cha mradi wao.

Usawa wa Kijinsia
Wabia wa Humanitarian Grand Challenge wanadhamiria kusimamia kanuni za usawa wa kijinsia kwenye miradi itakayofadhiliwa, kwa malengo yafuatayo: (1) kusimamia ushiriki sawa wa wanawake pamoja na wanaume kama watoa maamuzi katika kuunda maendeleo endelevu ya jamii zao; (2) kuwasaidia wanawake na wasichana kutambua haki zao kamili za binadamu; na (3) kupunguza hali ya kukosekana usawa wa kijinsia. Waombaji wa kike wanahimizwa sana kutuma maombi.

Haki za Binadamu na Ujumuishwaji
Wabia wa Humanitarian Grand Challenges wanaahidi kusimamia kanuni za haki za binadamu na ujumuishwaji kwenye vumbuzi zitakazopata ufadhili. Vumbuzi zinapaswa kuzingatia sauti za wale hasa wanaodunishwa kwenye muundo na utekelezaji wa uvumbuzi, ili kuhakikisha kwamba mahitaji yao yanashughulikiwa kwa usahihi.

Kanuni za Maadili
Wabia wa Humanitarian Grand Challenge wanaahidi kudumisha viwango vya hali ya juu vya tabia njema. Wavumbuzi wote watakaopewa ufadhili wanategemewa kuzingatia mwenendo wa kimaadili wa Grand Challenges Canada Sera za kanuni za maadili, kutobagua na heshima ili kuhakikisha miingiliano yote inafanywa kwa haki, utu, na kutokuwa na mingongano halisi au dhania ya kimaslahi. Wabia wa Humanitarian Grand Challenge wana sera isiyoruhusu kabisa unyanyasaji, uonevu, unyanyasaji wa kingono, udhalimu wa kingono au mienendo mingine isiyo sahihi.

2.10 UPATIKANAJI KIMATAIFA, UPATIKANAJI WA TAKWIMU NA MAADILI

Wabia wa Humanitarian Grand Challenge wanadhamiria kusimamia upatikanaji wenye tija kwa vumbuzi zinazofadhiliwa kwa walengwa wa kila mradi uliofadhiliwa, kuendelea usambazaji wa haraka na wa wazi wa gunduzi za utafiti na takwimu zinazoztokana na shughuli zilizofadhiliwa, na kuhakikisha kwamba utafiti uliofadhiliwa unaendeshwa kwa namna inayozingatia viwango husika vya maadili. Dhamira hizi zimejumuishwa kwenye Sera ya Upatikanaji Kimataifa, Sera ya Upatikanaji wa

Takwimu na Sera ya Maadili ya Grand Challenges Canada, ambazo zinapaswa kupitiwa kwa umakini na waombaji wote kabla ya kutuma maombi.

2.11 USIMAMIZI WA HATARI, USALAMA, KUPAMBANA NA UGAIDI, KUPAMBANA NA RUSHWA, KUPINGA RUSHWA

Mapendekezo ya mradili yatapaswa kuzingatia Sheria za Marekani, Uingereza, Uholanzi, Umoja wa Ulaya na Canada, ikiwa ni pamoja na sheria ya kupinga rushwa na kupinga ugaidi. Ufadhili hautatolewa kwa mtu au shirika lolote lililotajwa kwenye orodha ya kuwekewa vikwazo na Mabaraza ya Usalama ya Marekani, Uingereza, Uholanzi, Umoja wa Ulaya, Benki ya Dunia, Canada au Umoja wa Mataifa.

Wavumbuzi wote wanategemewa kusimamia hatari ya vifaa. Kwa miradi inayohusisha shughuli kwenye maeneo yasiyo salama, mapendekezo ya mradi yatapaswa kuwa na maelezo kuhusu usimamizi wa hatari ya usalama na ulinzi kwa kuwa zinawahusu watu pamoja na mali. Mapendekezo ya mradi yanapaswa pia kuelezea ni kwa namna gani rushwa itaepukwa, na ni hatua gani zitachukuliwa ili kuepuka upindishwaji wa msaada mbali na watu walioathirika.

2.12 MAMBO AMBAYO HATUTAYAFADHILI

1. Mbinu zinazotumia upepelezi wa masuala yanayohusiana na ulinzi, silaha, shurti au teknolojia kama hizo.
2. Sayansi ya ugunduzi, mipango ya kujenga uwezo, ufadhili unaondelea wa programu fulani au maendeleo ya miundimbinu.
4. Miradi inayohusisha kuanzisha ushahidi wa dhana ya vumbuzi ambazo haki za msingi za uvumbuzi zinamilikiwa na taasisi ya mhusika wa tatu, isipokuwa ama: (a) taasisi ya mshirika wa tatu imempatia mwombaji haki za kutosha za leseni ya uvumbuzi kiasi cha kuruhusu kutumiwa kwenye nchi husika, au (b) taasisi ya mhusika wa tatu iko tayari kusaini makubalino na Grand Challenges Canada ikiahidi kutii Sera ya Upatikanaji Kimataifa ya Grand Challenges Canada: www.grandchallenges.ca/wp-content/uploads/2015/11/Global-Access-Policy_25May2016_EN.pdf.

Vigezo vyote vinaweza kubadilika kadri wafadhili wapya wanavyojiunga na Challenge hii; habari mpya zitachapishwa kwenye sehemu ya “Maswali Yanayoulizwa Mara Nyingi” (FAQs) ya tovuti ya Humanitarian Grand Challenge https://humanitariangrandchallenge.org/apply-funding.

3. Shughuli na Vitu vya Kuwasilisha

Wavumbuzi waliofadhiliwa chini ya programu hii watategemewa kushiriki kwenye shughuli zifuatazo na kuwasilisha vitu muhimu vilivyoorodheshwa hapo chini, ili kuonesha maendeleo na mafanikio ya mradi:

1. Utoaji taarifa wa utendaji unaoweka mkazo kwenye matumizi ya fedha na matokeo yaliyopatikana. Utaratibu wa utoaji taarifa utakuwa kila baada ya miezi mitatu au sita, kulingana na tathimini yetu ya mradi na hatari za kitasisi.

2. Usambazaji wa maarifa katika muda mwafaka, kupitia mitandao ya kijamii, machapisho ya bure,

kuweka takwimu zenye utambulisho wa watu wanaolindwa kwenye vyanzo vinavyoweza kufikiwa na umma, taarifa kwa vyombo vya habari, mikutano, ushiriki wa wadau, n.k. utahitaji utambuzi wa wabia wa Humanitarian Grand Challenge.

3. Ripoti ya mwisho inayotoa taarifa ya matumizi ya fedha na ambayo inawasilisha tathimini ya wazi ya matokeo ya mradi husika. Tafadhali zingatia kwamba asilimia 5 ya fedha itashikiliwa kwa ufadhili wote chini ya programu hii, na itaachiwa kwa wavumbuzi baada ya kuwasilisha ripoti ya mwisho inayoridhisha na maelezo kamili ya gharama.

4. Mwendelezo wa habari mpya baada ya kupewa ruzuku kuhusu matokeo, upatikanaji kimataifa, upatikanaji wa takwimu na usimamizi wa haki za uvumbuzi kwenye vumbuzi zilizofadhiliwa.

Maelekezo kwa ajili ya utoaji ripoti yatatolewa kwa waombaji watakaoshinda. Taarifa za maendeleo zilizoandikwa pamoja na mazungumzo kupitia “teleconference” vitahitajika ili kukidhi matakwa ya utoaji ripoti. Mbali na shughuli zilizotajwa hapo juu, wavumbuzi watategemewa:

1. Kushiriki kwenye shughuli za umma za ushirikiano.

2. Kuchangia kwenye ajenga ya ujifunzaji kwa changamoto mahsusi, ikijumuisha kupitia kushiriki kwenye vikao, kama vile vikao vya mwaka vya Grand Challenges

Wavumbuzi watakaofadhiliwa wanapaswa kuhifadhi nyaraka muhimu za mradi, ikiwa ni pamoja na kumbukumbu za fedha, na zinaweza kukaguliwa na Grand Challenges Canada, Wizara ya Mambo ya Nje ya Uholanzi, DFID na/au USAID wakati wowote hadi kufikia Septemba 30, 2030; matakwa husika yataelezwa kwenye makubaliano ya ufadhili.

4. Sheria na Miongozo

Mapendekezo ya mradi yatakalowasilishwa hupitia mchakato wa mapitio wenye ngazi mbalimbali kabla ya Kamati Kuu ya Humanitarian Grand Challenges haijatoa mapendekezo ya ufadhili. Bodi ya Wakurugenzi wa Grand Challenges Canada ndiyo hutoa uamuzi wa mwisho wa ufadhili. Kwa maelezo zaidi: www.grandchallenges.ca/who-we-are/our-people/.

4.1 VIGEZO VYA SIFA

1. Waombaji wenye sifa wanajumuisha mashirika ya kijamii na taasisi nyingine zinazotambulika (k.m., mashirika yasiyopata faida na makampuni ya kupata faida) zilizoanzishwa na kusajiliwa kisheria, ambazo zinaweza kutekeleza kwa mafanikio shughuli husika kwenye eneo lao husika la kiufundi, na ambazo zinaweza kupokea na kusimamia fedha za ruzuku. Wafanyabiashara binafsi hawana sifa ya kupata ufadhili. Ofisi mkazi za Umoja wa Mataifa hazina sifa ya kutuma maombi. Katika uzoefu wetu wa nyuma, tumegundua kwamba mashirika ya kimataifa kama vile Umoja wa Kimataifa hayawezi kwa kawaida kukubaliana na vigezo na masharti ya makubaliano yetu ya ufadhili. Tunapendekeza sana kwamba badala yake mashirika haya yatume maombi kupitia shirika mbia mahalia lililo halali. Wafanyakazi wa ofisi ya Umoja wa Mataifa wanaweza kutenda kama washirika wa mradi.

2. Mradi unaweza kuwa na Kiongozi wa Mradi mmoja tu, ambaye anapaswa kuhusika na taasisi inayowasilisha mapendekezo ya mradi.

3. Kiongozi wa Mradi anaweza kuorodheshwa kwenye moja (1) tu ya maombi katika Ombi hili la Mapendekezo ya mradi. Taasisi inaweza kuwa mwombaji wa maombi mbalimbali, ilimradi maombi yote yana Viongozi tofauti wa Mradi.

4. Maombi ni lazima yajumuishe taarifa zote zinazohitajika. Maombi yaliyokamilka tu ndiyo yatakayozingatiwa na Kamati ya Mapitio.

5. Wabia wa Humanitarian Grand Challenge wanaweza, wakati wowote na kwa uamuzi wao binafsi, kurekebisha vigezo vya sifa kulingana na mwombaji mmoja mmoja, Viongozi wa Mradi na/au nchi zenye sifa ya kuomba, kwa namna ambayo marekebisho hayo hayatadhoofisha kwa kiasi kikubwa mchakato wa mapitio.

Tafadhali zingatia kwamba Grand Challenges Canada wanapaswa kuidhinisha mabadiliko yoyote kwenye shirika, taasisi au Kiongozi wa Mradi ambaye ni mwombaji kutokana na ruzuku iliyotolewa hapo awali.

4.2 MAELEKEZO YA MAOMBI

Kuwasilisha Maombi

Kuna vyanzo viwili tofauti ya uwasilishaji: kimoja kwa ajili ya mtaji na moja kwa ajili ya Mpito wa Kupima[3].

Maombi NI LAZIMA yawasilishwe kupitia Tovuti ya Jumuiya ta Grand Challenges Canada (gcc.fluxx.io).

Ili kuweza kuingia kwenye Tovuti husika, waombaji wanapaswa kwanza kuunda akaunti kwa kutumia kiungo kifuatacho: Unda akaunti. Mara baada ya kuunda akaunti, tafadhali subiri angalau siku moja (1) ya kazi ili Grand Challenges Canada washughulikie ombi la akaunti yako. Mara baada ya taarifa zako kushughulikiwa, utatumiwa baruapepe ya vitambulisho vya kuingia kwenye Tovuti ili uweze kuwasilisha maombi yako/Barua ya Kuelezea Nia. Kurudi kwenye Tovuti ya Jumuiya ili kuendelea kufanyai kazi maombi yako wakati wowote, tafadhali tembelea https://gcc.fluxx.io/.

Kwa msaada wa kiufundi, tafadhali tuma baruapepe kwenda fluxxsupport@grandchallenges.ca.

[3] Kwa Transaition to Scale, pamoja na wito huu wa wazi wa mapendekezo ya mradi, tuna haki pia ya kupata vumbuzi kupitia mwaliko wa moja kwa moja Waombaji wa Transition to Scale wataelezea uvumbuzi wao, ushahidi wa uthibitisho wa dhana, njia ya upanuzi na uendelevu, na matumizi pendekezwa ya fedha.

Waombaji wa mtaji watatakiwa kujibu mfululizo wa maswali kuhusu wazo lao la kivumbuzi, kusudi, malengo na shughuli, mbinu, mfumo kwa ajili ya kupima mafanikio, na bajeti.

Waombaji wa Mpito wa Kupima, kupitia barua ya Kuelezea Nia, wataelezea uvumbuzi wao, ushahidi wa dhana, kupima na uendelevu, na matumizi pendekezwa ya fedha.



Sanduku la Zana la Mvumbuzi (Toolbox)
Waombaji wanahimizwa kutembelea Sanduku la Zana la Mvumbuzi la mkondoni lililopo kwenye tovuti ya Grand Challenge Canada www.grandchallenges.ca/funding-opportunities/innovator-toolbox/, lenye vifaa vya kuwasidia watafiti na wavumbuzi kuendeleza Mapendekezo yao la mradi na kupanga ni kwa jinsi gani uvumbuzi wao utapanuka, utakuwa endelevu na kuwa na matokeo ya kimataifa. Tazama pia Tovuti ya Usawa wa Kijinsia www.grandchallenges.ca/funding-opportunities/gender/ for a set of gender equality tools.

Maswali
Tafadhali kwanza rejelea ukurasa wetu wa “Maswali yanayoulizwa Mara Nyingi” katika https://humanitariangrandchallenge.org/apply-funding. Maswali kuhusu Ombi hili la Mapendekezo ya Miradi ambayo hayajajibiwa kwenye ukurasa wetu wa hapo juu wa FAQ yanaweza kutumwa kwa baruapepe kwenda info@humanitariangrandchallenge.org kabla ya Julai 5, 2019.

Lugha
Maombi yanaweza kufanywa kwa lugha za Kiingereza na Kifaransa. Maombi kwa lugha nyingine yoyote yatatupiliwa mbali bila kupitiwa.

4.3 RATIBA ZA MUDA WA MAOMBI

Tukio	Tarehe Muhimu
Tarehe ya Mwisho ya Usajili Waombaji wanapaswa kuunda akaunti kupitia Tovuti ya Jumuiya ya Grand Challenges Canada (**gcc.fluxx.io**).	Julai 5, 2019
Tarehe ya Mwisho ya Maombi Maombi yanapaswa kuwasilishwa si zaidi ya saa 11:00 a.m North American Eastern Time Zone (15:00 GMT)	Julai 16, 2019
Mialiko ya kuwasilisha maombi kamili ya Mpito wa Kupima	
Taarifa ya hali ya maombi ya mradi wa msingi	Januari 2020
Tarehe inayotegemewa ya kuanza kwa miradi ya msingi	Juni 2020
Tarehe inayotegemewa ya kuanza kwa miradi ya Mpito wa Kupima	Septemba 2020

4.4 MCHAKATO WA MAPITIO

Mchakato wa mapitio ya Mapendekezo ya miradi kwa ufadhili wa miradi ya msingi pamoja na Mpito wa Kupima unahusisha Kuchunguza Sifa, Kuchunguza Ubunifu na Kamati ya Mapitio.

Uchunguzi wa Sifa
Grand Challenges Canada itachunguza maombi na Barua za Kuelezea Nia kwa mujibu wa vigezo vya sifa vilivyobainishwa kwenye Sehemu 4.1 Maombi ambayo hayatakidhi vigezo vya sifa yataondolewa kwenye shindano husika.

Uchunguzi wa Uvumbuzi
Maombi ya Mtaji/Barua za Kuelezea Nia za Mpito wa Kupima yatawekewa alama ndani dhidi ya vigezo hapo chini, kwa kutumia majibu ya maswali ya maombi/Barua za Kuelezea Nia kwenye sehemu ya “Ufupisho wa Mradi” Vigeo hivyo viwili vinapewa uzito sawa

Zingatia: Uchunguzi wa Uvumbuzi hautatathimini utendekaji au ubora wa Mapendekezo ya mradi. (Tathimini hiyo itafanyika katika hatua ya usoni kwenye mchakato.) Miradi itakayokosa uvumbuzi na umuhimu itaondolewa kwenye shindano husika kwenye hatua hii.

Vigezo vya Uchunguzi wa Uvumbuzi:

1. **Uvumbuzi**
   - Je, wazo lililopendekezwa limeelezewa kwa usahihi?
   - Je, uvumbuzi husika unawakilisha zaidi ya maboresho ya ziada juu ya mbinu zilizopo sasa?

2. **Umuhimu**
   - Je, ufumbuzi uliopendekezwa unashughulikia tatizo mahsusi chini ya Human Grand Challenge, kama ilivyoelezwa kwenye Sehemu 2.1 n 2.2?
   - Je, ufumbuzi uliopendekezwa unawalenga watu walio kwenye mazingira magumu ambao ni vigumu kufikiwa na wameathiriwa na mapigano, kama ilivyoelezwa kwenye Sehemu 2.4?

Kwenye ngazi ya Mpito wa Kupima, Barua za Kuelezea Nia ambazo zinahamasisha zitapewa mwaliko wa kuwasilisha maombi kamili ya Mpito wa Kupima kwa ajili ya umakini na Kamati ya Mapitio.

Uchunguzi wa Kamati ya Mapitio
Kwa mapendekezo ya miradi yatakayofaulu uchunguzi wa Sifa na Uvumbuzi, Kamati ya Mapitio ya wapitiaji wa kisayansi, kijamii na kibiashara, ikiwa ni pamoja na wataalamu wa masuala ya kibinadamu na watu walioathiriwa, watashauri juu ya ustahili wa mapendekezo ya miradi, kulingana na vigezo vya tathimini kwenye Sehemu 4.4 na 4.5.

Mapendekezo ya ombi la miradi yatapangwa kwenye orodha nne, moja kwa kila eneo la nia kama ilivyoainishwa kwenye Sehemu 2.2. Kulingana na ubora wa mapendekezo ya mradi lililopokelewa, wabia wa Humanitarian Grand Challenge kuwa na haki ya kupunguza mkazo kwa eneo moja au zaidi ya maeneo hayo manne.

Mpito wa Kupima Umakini
Mapendekezo ya mradi ya Transition to Scale ytakayoonekana kuwa na tija yatapitia mchakato wa kina wa kujiridhisha kwa uwezekano wa matokeo, shughuli, fedha, vigezo vya kiufundi, milikibunifu, ushirikiano, usawa wa kijinsia, uendelevu wa mazingira, na haki za binadamu na ujumuishwaji. (Tazama Sehemu 4.6 kwa vigezo kamili vya tathimini ya Mpito wa Kupima.) Umakini unaweza kuhusisha mahojiano na waombaji, wabia, washauri na wadau wa upande wa tatu.

Mapendekezo ya ufadhili yatatolewa kulingana na utafiti kutoka kwenye mchakato wa kina wa umakini. Grand Challenges Canada, kwa mujibu wa kesi kwa kesi na kwa ushauri wa wabia wa Humanitarian Grand Challenge, wanaweza kuchagua kupendekeza waombaji ambao hawakidhi Vigezo vyote vya Uwekezaji kwa ajili ya ufadhili wa kiasi kidogo ili kuweka mkazo kwenye maeneo machache muhimu yanayohitajika kwa mpito wa kupima. Ili kutaarifu utoaji maamuzi wa mwisho, Grand Challenges Canada itaandaa mapendekezo yanayoelezea uhalali wa ufadhili na itafanya kazi na mvumbuzi kuboresha na kuunda uwekezaji wakati wa mchakato wa umakini. Kwa nafsi yake, Grand Challenges Canada inaweza kuamua kutowakubali waombaji kwa ajili ya uamuzi wa ufadhili; kutokana na taarifa zinazotokana na umakini au udhaifu mwingine wowote utakaoonekana kwenye Vigezo vya Uwekezaji.

Maamuzi ya Ufadhili (Mtaji)
Kutokana na matokeo ya kamati ya mapitio, Kamati kuu ya Humanitarian Grand Challenge itawasilisha mapendekezo ya ufadhili kwa Bodi ya Wakurugenzi wa Grand Challenges Canada, ambayo nayo itatoa maamuzi ya mwisho kwa nafsi yake kama Bodi, ikiwa ni pamoja na haki zake

binafsi zilizoainishwa kwenye Sehemu 4.14. Miradi iliyochaguliwa na Kamati ya Mapitio tu kuwa inafadhilika ndiyo inaweza kupendekezwa kwa ufadhili. Umakini unapaswa kuzingatiwa kwa miradi yote iliyopendekezwa na Kamati ya Mapitio kwa ajili ya ufadhili. Kutokana na matokeo ya Kamati ya Mapitio au mchakato wa umakini, maboresho kwenye mapendekezo ya mradi yaliyopendekezwa, muundo, kiasi, aina ya ufadhili na usimamizi vinaweza kuhitajika wakati wa mazungumzo ya makubaliano ya ufadhili.

(Mpito wa Kupima PEKEE)
Maamuzi ya mwisho ya ufadhili yanafanywa na Bodi ya Wakurugenzi ya Grand Challenges Canada. Mapendekezo kwa ajili ya ufadhili kwa Bodi ya Wakurugenzi yanatolewa na Kamati ya Uwekezaji baada ya kupitia mapendekezo ya wafanyakazi (Kutokana na mapitio ya nyaraka za maombi zilizotolewa na mvumbuzi na umakini wa ziada) na taarifa nyingine zilizopo, kama vile mahojiano mafupi na mvumbuzi.

4.5 VIGEZO VYA TATHIMINI

Matokeo

- Je, ufumbuzi uliopendekezwa una uwezekano wa kutengeneza msaada wa kuokoa maisha au kuboresha maisha kwa watu walio kwenye mazingira magumu kwenye maoneo ambayo ni magumu kufikika na kwenye muktadha wa kuathiriwa na mapigano? **(Mtaji PEKEE)**
- Je, ushahidi wa dhana umedhihirishwa kwa ajili ya ufumbuzi unaopendekezwa? **(Mpito wa Kupima PEKEE)**
    - Ushahidi wa dhana: ushahidi uliotolewa kwenye mazingira yanayodhibitiwa au yaliyozuiliwa ya (1) usaidizi ulioboreshwa, utegemezi mdogo kuhusu uagizaji, na/au upungufu wa vikwazo vingine muhimu katika kupata usaidizi kwenye muktadha unaotokana na mapigano; na (2) uhitaji wa ufumbuzi
- Je, ufumbuzi unaopendekezwa ni sahihi kwa utekelezaji mpana kwenye mazingira yenye mapigano?
- Je, wazo linalopendekezwa linahusika kwa watu husika walio kwenye mazingira magumu kwenye maeneo yaliyoathiriwa na mapigano na linaweza kushughulikia ukosefu wa usawa?

Uvumbuzi Fungamano

- Je, uvumbuzi husika ni wa kipekee?
- Je, ni kwa namna gani wazo linalopendekezwa linajumuisha kwa ufasaha uvumbuzi wa kisayansi/kiteknolojia, kijamii na kibiashara?
- Je, ni kwa namna gani watu walioathiriwa watashirikishwa kwa ufanisi katika kuunda, kujaribu na kurudia tena uvumbuzi unaopendekezwa?

Mpango wa Utekelezaji wa Mradi

- Je, mpango wa utekelezaji wa mradi umeundwa kuonesha ushahidi wa dhana ya wazo ndani ya muda na rasilimali zilizopo? **(Mtaji PEKEE)**
    - Ushahidi wa dhana: ushahidi uliotengenezwa kwenye mazingira yanayodhibitiwa au yaliyozuiliwa ya (1) usaidizi ulioboreshwa, utegemezi mdogo juu ya uagizaji, na/au upungufu wa vikwazo vingine muhimu katika kupata usaidizi kwenye muktadha unaotokana na mapigano; na (2) uwezekano wa kutekelezwa kwa upana kwenye muktadha mwingine.

- Je, pendekezo la mradi linadhihirisha mpango ulioandaliwa vizuri kwa ajili ya kupima na uendelevu, ikiwa ni pamoja na dhamira kutoka kwa wadau na wabia zinazohitajika ili kufanikiwa kwenye njia ya kupima na uendelevu? **(Mpito wa Kupima PEKEE)**
- Je, kuna uhusiano na sekta binafsi ambao utaongeza uwezekano wa mafanikio?
- Je, mpango wa kufuatilia na kutathimini matokeo ni thabiti vya kutosha, ili kuweza kupata hitimisho sahihi kufikia mwisho wa ufadhili?
- Je, ni kwa namna gani pendekezo la mradi linazingatia kwa ufasaha usawa wa kijinsia, uendelevu wa mazingira, na haki za binadamu na ujumuishwaji?
- Je, kuna ushahidi uliotolewa kuashiria uwezekano wa mafanikio, na tathimini ya kina ya hatari za mradi, hatari za rushwa, hatari za kuhamisha msaada sehemu nyingine, hatari za usalama na ulinzi na mikakati husika ya kupunguza mambo hayo? (Hii inapaswa kujumuisha faragha na ufaragha wa takwimu za watu walioathiriwa, ikiwezekana, na kuzingatia wafanyakazi, watu walioathiriwa, jumuiya yote kwa ujumla na wadau wengine.)

Uwezo wa Uongozi wa Kutetea Mabadiliko

- Je, Kiongozi wa Mradi na wajumbe muhimu wa timu wana dhamira na sifa ya uongozi unaohitajika kuleta kupima fumbuzi?
- Je, Kiongozi wa Mradi anayependekezwa na/au wajumbe muhimu wa timu wamepata mafunzo sahihi, wana uzoefu na kuwa kwenye nafasi ya kutekeleza kazi inayopendekezwa?
- Je, ni kwa namna gani Kiongozi wa Mradi na/au wajumbe muhimu wa timu wamedhihirisha kwa kiwango kikubwa uwezo wa kutumia utaalamu wa sekta binafsi?
- Je, Kongozi wa Mradi na/au wajumbe muhimu wa timu wamedhihirisha uwezo wa kuelewa na kukidhi mahitaji ya watu walioathiriwa kwenye muktadha husika?

Thamani ya Jitihada

- Je, wigo wa kazi inayopendekezwa, uwezo wa timu ya Mradi husika, na fedha zilizoombwa ni halali na sahihi kulingana na malengo yanayopendekezwa ya pendekezo la mradi?
- Je, pendekezo la mradi linawakilisha matumizi fanisi na zingativu ya rasilimali?

4.6 VIGEZO VYA TATHIMINI– KWA AJILI YA KUJIRIDHISHA KUHUSU MAOMBI YA TRANSITION TO SCALE

Maombi kamili yatakayoitwa kwa ajili ya ufadhili wa Mpito wa Kupima yatatathiminiwa na Grand Challenge Canada na kamati yake ya Uwekezaji, ikiwezekana, kulingana na vigezo vifuatavyo:

- **Uvumbuzi Fungamano** – Je, uhusiano wa matumizi ya uvumbuzi kisayansi/kiteknolojia, kijamii na kibiashara kuongeza uwezekano wa kupima na kupata matokeo endelevu kwenye kupima ni thabiti kiasi gani?
- **Matokeo** – Je, kuna uwezekano wa maisha ya siku za usoni kuokolewa na kuboreshwa?
- **Ujasiriamali** – Je, timu ina uwezo, stadi na sifa ya kutekeleza dira na mkakati wao unaopendekezwa
- **Ubia Fanisi** – Je, timu ina ushirikaino wa kutosha wa kimkakati na/au ubia utakaowezesha kupima uvumbuzi husika? Kwenye ngazi ya mpito wa kupima, ushiriki na sekta binafsi unapaswa kuzingatiwa. Ufadhili linganifu utachukuliwa kwa upendeleo kama ishara thabiti ya ahadi kutoka kwa wabia wa kimkakati.
- **Uendelevu** – Je, kuna njia fanisi ya kufikia uendelevu wa kifedha kupitia chaneli binafsi na/au za umma (bila ya kuomba fedha zaidi kutoka kwa wabia wa Humanitarian Grand Challenges)?

- **Wigo Unaotarajiwa wa Kazi** – Je, wigo wa mpango unaopendekezwa na fedha zinazoombwa ni halali na sahihi kulingana na malengo yanayopendekezwa kwa ajili ya Mpito wa Kupima?
- **Utekelezaji** – Je, mpango unaopendekezwa unaweza kutekelezwa kwa ufanisi, kuendelezwa na kusaidiwa kifedha wakati wa kipindi cha ufadhili cha Mpito wa Kupima?
- **Uzingatiaji wa Maadili** – Je, mpango unaopendekezwa unazingatia utendaji bora wa kimaadili?
- **Uendelevu wa Mazingira, Usawa wa Kijinsia, Haki za Binadamu na Ujumuishwaji?**

    1. Uendelevu wa Mazingira – Je, pendekezo la mradi linaendana na dhamira ya Grand Challenges Canada ya kuhakikisha inazuia madhara kwenye mazingira?
    2. Usawa wa Kijinsia – Je, pendekezo la mradi linaendana na dhamira ya Grand Challenges Canada ya kusimamia kanuni za usawa wa kijinsia?
    3. Haki za Binadamu na Ujumuishwaji – Je, pendekezo la mradi linaendana na dhamira ya Grand Challenges Canada ya kusimamia kanuni za Haki za Binadamu na Ujumuishwaji?
- **Upatikanaji Kimataifa na Upatikanaji wa Takwimu**
    1. Milikibunifu – Je, Mvumbuzi amefuata masuaal ya kisheria na/au kusimamia haki za uvumbuzi kwa namna inayomwezesha mvumbuzi kutii Sera ya Upatikanaji Kimataifa na Sera ya Upatikanaji wa Takwimu za Grand Challenges Canada, na kuwapatia Grand Challenges Canada haki za uvumbuzi chini ya Makubaliano ya Upatikanaji Kimataifa?
    2. Upatikanaji Kimataifa – Je, Mpango Kazi wa mvumbuzi unaonekana kuwezesha upatikanaji wa msingi wa uvumbuzi kwa walengwa, hasa wale walio kwenye mazingira magumu, ikiwa ni pamoja na watu wenye ulemavu?
    3. Upatikanaji wa Takwimu – Je, Mpango Kazi wa mvumbuzi unazingatia kuchapisha na/au kusambaza matokeo na takwimu kwa namna iliyo wazi na kwa wakati mwafaka?

4.7 VIGEZO VYA KIFEDHA NA GHARAMA STAHIKI

Gharama zinazohusiana moja kwa moja na utekelezaji wa mradi ni sahihi kulingana na Maelekezo ya Grarama Sahihi na Zisizo Sahii.

Gharama Zisizo za Moja kwa Moja/za Ziada
Gharama zisizo za moja kwa moja/za ziada **si stahiki**

4.8 VIGEZO VYA MALIPO

1. Malipo ya awali: Malipo ya awali sawa na makadirio ya mahitaji ya mzunguko wa fedha kwa gharama halali zilizotabiriwa kwa kipindi cha kwanza yatalipwa baada ya kusaini Makubaliano. Malipo yanayofuata yatalipwa kila robo kulingana na makadirio ya mahitaji ya mzunguko wa fedha kwa Gharama Stahiki. Malipo ya awali yanayofikia asilimia 5 yatashikiliwa kwenye kiasi kilichotabiriwa.

2. Maombi yote ya fedha ya awali na ripoti za kifedha zitasainiwa na mkaguzi mwandamizi mwenye uthibitisho wa kitaaluma wa uhasibu.

3. Baki ya Malipo: Malipo ya awali hayawezi kukidhi zaidi ya vipindi viwili na hakuna wakati

ambao kutakuwa na malipo ambayo hayajalipwa ya kukidhi mahitaji ya mzunguko wa fedha ya zaidi ya vipindi viwili. Kwa mfano, kabla malipo ya awali hayajalipwa kwa kipindi cha tatu, kipindi cha kwanza kinapaswa kutolewa hesabu zake.

4. Akaunti Tofauti ya Benki na Riba Inayotokana na Malipo ya Awali: Akaunti tofauti ya benki, inayoongezeka riba, itafunguliwa kwa ajili ya mradi husika.

5. Malipo ya mwisho yatategemea masharti yafuatayo:
    a. Mradi umekamilika kulingana na Makubaliano.
    b. Grand Challenges Canada imepokea na kuikubali ripoti ya mwisho.
    c. Grand challenge Canada imepokea cheti kinachobainisha kwamba wajibu wa kifedha kwa wafanyakazi, wahandisi au wasambazaji kwa mujibu wa mchango wa Grand Challenges Canada kwa mradi husika umetekelezwa kikamilifu.

4.9 UKAGUZI

Wavumbuzi watakaofadhiliwa wanaweza kukaguliwa na Grand Challenges Canada au yeyote wa wabia wake, wakati wowote hadi kufikia Septemba 30, 2030, na wanapaswa kuhifadhi kumbukumbu za mradi kwa kipindi hicho, ambazo zote kwa pamoja zitadhihirishwa katika makubaliano ya ufadhili.

4.10 NYARAKA ZA KUWAKILISHA NA ILANI YA FARAGHA

Nyaraka zote za maombi zitakazotumwa kwa Grand Challenges Canada kuhusiana na Ombi hili la Mpendekezo ya mradi (kwa pamoja, “Nyaraka za Kuwasilisha”) zinaweza kushirikishwa kwa Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID), Ofisi ya Msaada wa Maafa kwa Nchi za Nje (OFDA), Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (DFID) Wizara ya Mambo ya Nje ya Uholanzi na/au na wabia wengine, na labda kutangazwa kwa umma. Kwa kuwasilisha Nyaraka zozote za Kuwasilisha kwa Grand Challenge Canada, kila mwombaji anawapatia Grand Challenges Canada, DFID, Wizara ya Mambo ya Nje ya Uholanzi, na USAID Kimataifa, leseni yote, isiyo na mipaka na ya bure ya kutumia, kubainisha, kuzalisha upya, kuandaa kazi za kuiga, kusambaza nakala kwa umma, na kuendesha hadharani na kuonesha hadharani, Nyaraka Za Kuwakilisha, kwa namana yoyote na kwa madhumuni yoyote, na kuruhusu wengine kufanya hivyo kwa vigezo hivyo hivyo. Hii inahusisha kushirikishana mapendekezo ya miradi kwa mifuko ya hisani mingine ya Challenge na zawadi ambayo huendeshwa na mashirika ya kielimu, sekta binafsi, kibinadamu na Umoja wa Mataifa.

Mapendekezo ya miradi yatapaswa kufanyiwa mapitio ya nje na wataalamu wa kujitegemea wa maudhui husika na wanaoweza kuwa wafadhili wenza (matokeo ambayo yatakuwa siri), pamoja na uchambuzi utakaofanywa na wabia wa Humanitarian Grand Challenge.

Tafadhali zingatia kwa umakini taarifa zinazojumuishwa kwenye Nyaraka za Kuwasilishwa. Kama una mashaka yoyote kuhusu busara ya kutotoa taarifa za siri au za kipekee (ikiwa ni pamoja na taarifa zinazohusiana na vumbuzi), tunapendekeza uwasiliane na mwanasheria wako kwa ajili ya kuchukua hatua zozote unaozooa zinafaa ili kulinda milikibunifu yako.

Unaweza kuamua kuzingatia iwapo taarifa hizo ni muhimu kwa kutathiminiwa na kuwasilishwa na iwapo taarifa ambazo ni za jumla, zisizo za siri zinaweza kutosha kama mbadala wa malengo haya.

Grand Challenges Canada inakanusha wazi wazi kuwajibika kwa namna yoyote kutakokea kutokana na kutoa taarifa za siri zilizomo kwenye Nyaraka za Kuwakilisha.

4.11 HATI YA IDHINI

Kwa kutoa Nyaraka yoyote ya Kuwasilishwa, waombaji wanabainisha na kuthibitisha kwamba wana haki ya kutoa taarifa hizo zilizowasilishwa na kutoa leseni husika hapo juu.

Waombaji wenye maswali kuhusiana na maudhui ya Nyaraka zao za Kuwasilishwa wanaweza kuwasiliana nasi kwa baruapepe kwa info@humanitariangrandchallenge.org.

4.12 HAKI ZA UVUMBUZI

Ufumbuzi unaoungwa mkono na programu hii uinahusisha teknolojia, huduma, muundo wa biashara, maarifa na/au bidhaa za kivumbuzi za kuendeleza utendaji wa kibinadamu kwenye muktadha ulioathiriwa na mapigano. Ili kuhakikisha ufikiwaji sahihi wa walengwa, maendeleo yenye mafaniko na utoaji wa fumbuzi hizi yanaweza kuhitaji ushiriki wa, uungwaji mkono wa na/au ushirikiano na mashirika mbalimbali, ikiwa ni pamoja na sekta binafsi, taasisi za serikali na elimu na/au taasisi za kufanya utafiti zisizo za kupata faida. Vivyo hivyo, lengo la programu hii ni kuunga mkono uundwaji wa ushirikiano sahihi ambao ni muhimu ili kukidhi mahitaji haya ya haraka ya kiafya kimataifa.

Waombaji watakaoshinda wana haki ya umiliki wa haki za uvumbuzi kwa vumbuzi zitakazofadhiliwa, ikiwa ni pamoja na haki zinatokana na matokeo ya miradi inayofadhiliwa. Hata hivyo, Grand Challenges Canada inalenga kuhakiksha kwamba haki zozote za uvumbuzi zinatumiwa na kusimamiwa kwa namna inayoendana na ufikiwaji wa malengo ya programu hii. Sera ya Upatikanaji Kimataifa ya Grand Challenges Canada itakuwa mwongozo wa mbinu yetu kwa milikibunifu, na tunawasihi waombaji wote kuzingatia utayari wao wa kuwasilisha maombi kwa kutii Sera ya Upatikanaji Kimataifa ya Grand Challenges Canada.

Waombaji watakaoshinda watahitajika kudhamiria kutii Sera ya Upatikanaji Kimataifa ya Grand Challenges Canada na kusaini Makubaliano ya Upatikanaji Kimataifa, pamoja na Kanuni Kiongozi, zinazohusika kwa fumbuzi za kivumbuzi na matokeo ya mradi unaoungwa mkono na programu hii. Makubaliano ya Upatikanaji Kimataifa itatoa leseni isiyo ya kipekee kwa haki za uvumbuzi kwa vumbuzi zinazofadhiliwa (ikiwa ni pamoja milikibunifu ya nyuma) inayoruhusu Grand Challenges Canada na wabia wake wa ufadhili na wenye leseni kutekeleza na kusambaza bidhaa, michakato, maarifa au fumbuzi kwenye nchi za kipato cha chini na cha kati ambazo waombaji au wabia wao hawana uwezo wa kufika kwa urahisi. Waombaji wanapaswa kuzingatia kwamba Grand Challenges Canada wanaweza kuhitajika kutoa leseni au kutoa haki za usambazaji kwa wabia wa ufadhili, au mtu mmoja au zaidi aliyeteuliwa na wabia wa ufadhili. Waombaji wanapaswa kuzingatia kwamba dhamira hizo hapo juu za upatikanaji kimataifa zitakuwepo hadi mwisho wa shughuli za mradi.

4.13 UPATIKANAJI WA TAKWIMU

Grand Challenges Canada inadhamiria kuboresha matumizi ya takwimu ili kubadilisha maarifa kuwa fumbuzi za kuokoa maisha. Ili kutimiliza lengo hili, ni lazima takwimu zipatikane kwa wigo mpana na kwa haraka kwa jumuiya ya utafiti ya Grand Challenges Canada na jumuiya yote ya masuala ya kibinadamu kwa njia ya upatikanaji wa takwimu unaozingatia maadilii. Kwa mujibu wa upatikanaji kimataifa, upatikanaji wa takwimu unawakilisha ufafanuzi wa kanuni ya pili kiongozi ya Sera ya

Upatikanaji Kimataifa, inayosema kwamba maarifa yaliyopatikana kupitia ugunduzi ni mapana, na mapema kadri iwezekanavyo, yasambazwe kati ya miradi inayohusiana na kwenye jumuiya ya kimataifa ya kisayansi.

Kwa maelezo mafupi, “takwimu” hurejelea mkusanyiko wa taarifa zinazohusiana, ambazo ni za mwisho, zilizoorodheshwa kwa wingi na ubora zinazolinda utambulisho wa watu binafsi, na zinazoendana, kama vile metadata, codebooks, kamusi za takwimu, madodoso na itifaki.

Grand Challenges Canada inatambua tamani ya milikibunifu na mauzo, na faida za matumizi ya kwanza na ya baadaye ya takwimu, lakini si matumizi ya muda mrefu au ya kipekee. Katika hali fulani, ulinzi, sheria au kanuni za milikibunifu zinaweza kuchelewesha au kuzuia upatikanaji wa takwimu. Katika hali kama hizo, mpewa ruzuku atatoa sababu halali ya kuthibitisha ondoleo la haki kwa sehemu au kikamilifu la mahitaji ya upatikanaji wa takwimu.

4.14 HAKI ZA GRAND CHALLENGES CANADA

Ombi hili la Mapendekezo ya Miradi ni sehemu ya programu ya wazi ya kupewa ruzuku. Uwasilishaji wa maombi hautengenezi uhusiano wa kimkataba kati ya mwombaji na Grand Challenges Canada.

Grand Challenges Canada ina haki, kwa uamuzi wake wa kipekee na bila ya kutoa taarifa, ya:

1. Kusitisha Ombi hili la Mapendekezo ya miradi wakati wowote na kwa sababu yoyote.
2. Kubadilisha na kutoa upya Ombi la mapendekezo ya mradi wakati wowote na kwa sababu yoyote. Ombi hili la Mapendekezo ya miradi ni halali kuanzia Mei 21, 2019, na linachukua nafasi ya Ombi lingine lolote la Mapendekezo ya mradi ya aina hii yaliyotolewa huko nyuma. Vigezo na masharti vya Ombi hili la Mapendekezo ya miradi vinahusika kwa maombi yote yaliyowasilishwa kuanzia Mei 21, 2019 na kuendelea na linaweza kubadilisha na Ombi lililopitiwa la Mapendekezo ya miradi katika siku za usoni. Tunapendekeza kukagua mapitio yoyote kwenye Ombi la Mapendekezo ya miradi kabla ya kuwasilisha maombi yako.
3. Kukubali au kukataa maombi yoyote yaliyo tofauti kwa kuwa hayakidhi vigezo vya sifa, hayaendani na maelekezo ya gharama zinazoruhusiwa.
4. Kutotoa tuzo kwa maombi husika kwa mujibu wa utendaji wa nyuma wa ruzuku au mradi wa Grand Challenges Canada, au kutokana na tuzo ya ruzuku kwa mwombaji kwa utafiti sawa au unaofanana na mmoja wa wabia wa Grand Challenges Canada au taasisi washirika.
5. Kuondoa sifa ya maombi yoyote kwenye hatua yoyote ambapo kutakuwa na kiashiria kwamba mapendekezo ya mradi, kwa namna yoyoteli, limenakiliwa kutoka mahali fulani.
6. Kukubali au kukataa ombi lolote au maombi yote, licha ya alama ya maombi hayo husika, kulingana na vigezo vya tathimini, kwa kutoa au bila kutoa maelezo.
7. Kutoa tuzo kwa maombi yenye kiasi tofauti cha ufadhili, vipindi tofauti na/au hali tofauti kuliko zile zilizaoinishwa hapo juu.
8. Kuthibitisha taarifa zilizotolewa na waombaji kupitia mtafiti wa kujitegemea au kwa kuwasiliana na wahusika upande wa tatu wanaoaminika na Grand Challenges Canada, na kutumia taarifa hizo kutaarifu uamuzi wa ufadhili wa Grand Challenge Canada.
9. Kutoa ruzuku kwa kushirikiana na wabia wa ufadhili. Hii inaweza kuhusisha makubaliano mengine kabisa ya ruzuku kwa kila taasisi (k.m., mmoja kutoka kwa Grand Challenges Canada na mwingine kutoka kwa taasisi mbia), pamoja na maingizo tofauti ya fedha. Ufadhili wowote wa aina hii unaweza kuwa chini ya vigezo na masharti tofauti na vile vilivyoelezwa kwenye waraka huu. Grand Challenges Canada ina haki ya kujadili mahitaji/vigezo na masharti yoyoye ya ziada ya Milikibunifu ya wabia wowote wa Humanitarian Grand Challenge.

4.15 HAKIKA ZA UTAFITI

Kama ilivyoelezewa hapo juu kwenye Sehemu 2.10, ni sera ya Grand Challenges Canada kwamba utafiti unaohusisha binadamu, utafiti wa wanyama na utafiti unaopaswa kukidhi mahitaji ya ziada ya kisheria ni lazima uendeshwe kwa mujibu wa viwango vya juu kabisa vya maadili vinavyotambulika kimataifa. Ili kuweza kupata ufadhili kutoka Grand Challenges Canada, kwanza kabisa na katika kipindi chote cha mradi wa utafiti, watafiti wanapaswa kuthibitisha na kuzingatia uzingatiaji kwa kanuni kiongozi za maadili na viwango vilivyoainishwa hapo chini:

1. Utafiti unaohusisha washiriki ambao ni binadamu unapaswa kuendeshwa kwa namna inayodhihirisha, inayolinda na kudumisha heshima kwa watu, kujali ustawi wa watu, familia na jumuiya, na haki zao.
2. Utafiti unaohusisha wanyama unapaswa kuendeshwa kwa namna ambayo itahakikisha kujali utu wao.
3. Baadhi ya shughuli za utafiti, ikiwa ni pamoja na, lakini haziishii tu katika tafiti za "*recombinant DNA*", bayohatari na viumbehai waliobadilishwa vinasaba, huweza kuhusisha sheria na usimamizi zaidi.

Kama inavyohusika kwa mradi mmoja mmoja, Grand Challenges Canada watahitaji kwamba, kwenye kila eneo ambalo sehemu yoyote ya mradi inafanyika (ama na taasisi yako au mpewa ruzuku wa ngazi ya chini au mhandisi wa ngazi ya chini), lazima idhini zote za kisheria kwa shughuli zinazoendeshwa zipatikane kabla ya kuanza shughuli husika inayosimamiwa kisheria. Tutakuhitaji zaidi ukubali kwamba hakuna fedha zitakazotumika kufanyia wanadamu utafiti hadi pale idhini husika kutoka kwa vyombo vya kisheria na maadili itakapopatikana. Kwa maelezo zaidi, tafadhali tazama Sera ya Maadili ya Grand Challenges Canada.

KIAMBATISHO A

KUTOA TAARIFA YA MATOKEO

Viashiria Muhimu
Ikiwa mradi wako umefadhiliwa, utahitajika kutoa ripoti juu ya idadi ya matokeo na matokeo ya awali, ikiwa ni pamoja na masuala hayo yaliyofupishwa hapo chini; zingatia kwamba hii si orodha kamili, na matokeo na matokeo ya awali yataamuliwa na timu ya mradi kwa kushirikiana na Grand Challenges Canada.

Matokeo ya Mwisho
Matokeo ya mwisho yanarejelea matokeo ya muda mrefu yaliyotakana na uvumbuzi husika. Matokeo ya mwisho yanapaswa kufikika na kupimika kufikia mwisho wa kipindi cha ufadhili. Matokeo ya mwisho ambayo Humanitarian Grand Challenges inayalenga ni idadi ya **maisha yaliyoboreshwa;** na idadi ya **maisha yaliyookolewa.**

Matokeo ya Kipindi cha Kati
Matokeo ya Kipindi cha Kati ni mabadiliko ya nusu ya kipindi cha mradi yaliyotokana na uvumbuzi husika. Matokeo hayo yanapaswa kufikika na kupimika ndani ya vikwazo vya muda na rasilimali za mradi, na kuhusishwa moja kwa moja kwenye matokeo ya mradi husika. Matokeo ya kipindi cha kati ambayo Grand Humanitarian Challenge inayalenga ni:

- Idadi ya watu walioathiriwa wanaotumia uvumbuzi husika.
- Idadi ya wafanyakazi wanaotumia uvumbuzi husika (“wafanyakazi” ni watoa huduma au wafanyakazi wa misaada ya kibinadamu wanaotumia uvumbuzi husika kuokoa au kuboresha maisha kwenye jumuiya iliyolengwa).

Matokeo ya Papo Hapo
Matokeo ya papo hapo ni mabadiliko ya muda mfupi yanayotokana na uvumbuzi husika. Matokeo haya yanapashwa kupimika na kufikika mapema iwezekanavyo baada ya mradi kuwa umetekelezwa, na yanapaswa kuhusishwa moja kwa moja na matokeo ya mradhi husika. Mifano ya matokeo ya papo hapo ambayo Humanitarian Grand Challenges inayalenga ni:

- Idadi ya watu walioathiriwa ambao wamefikiwa kupitia shughuli za ufikiaji na utambuzi.
- Idadi ya wafanyakazi waliofikiwa kupitia shughuli za ufikiaji na utambuzi.
- Idadi ya wafanyakazi waliopata mabadiliko katika maarifa au stadi kutokana na mafunzo juu ya uvumbuzi husika.

Matokeo ya Awali
Matokeo ni vizao au huduma zilizozalishwa, zilizoandaliwa na kutekelezwa moja kwa moja kama sehemu ya uvumbuzi husika. Mifano ya matokeo ambayo Humanitarian Grand Challenge inayalenga ni:

- Idadi ya wafanyakazi waliopata mafunzo ya uvumbuzi husika
- Idadi na aina ya shughuli za ufikiaji na utambuzi zilizofanyika
- Idadi ya ajira zilizotengenezwa kutokana na uvumbuzi husika.